# CLASS 8 MID TERM 3 DECEMBER 2021
# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Jambazi ni mtu ambaye__1__uhai wa wengine. Tamaa__2__ni kujipatia mali__3__hata endapo katika kufanya hivyo ataangamiza maisha ya wengine. Huyu ni mtu ambaye ana__4__wa maadili. Haelewi kuwa tamaa mbele mauti nyuma. Binadamu wameamua__5__ili kupambana na adui huyu. Watu hushirikiana kwani wanaelewa kuwa__6__mafanikio yatapatikana tukiwapata askari wa kutosha wa__7__ usiku. Watu watendeane mema ili wapendane na kuaminiana kwani hisani iandamane na matendo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** hadhamini | **B.** haamini | **C.** hathamini | **D.** hatamani |
| **2.** | **A.** lake | **B.** yake | **C.** chake | **D.** wake |
| **3.** | **A.** mengi | **B.** mingi | **C.** wengi | **D.** jingi |
| **4.** | **A.** upotovu | **B.** upotovu | **C.** utofu | **D.** utovu |
| **5.** | **A.** kujiamini | **B.** kujihami | **C.** kujiami | **D.** kujiharibu |
| **6.** | **A.** kulenga si kuvuma | **B.** pavumapo si kazi kudaminka | **C.** mkataa wengi ni mchawi | **D.** mhini na mhiniwa njia yao ni moja |
| **7.** | **A.** kupiga doria | **B.** kupiga makasia | **C.** kupiga miguu | **D.** kupiga kwata |

Watu wale__8__walipoona tukiwa wajinga kama__9__. Tulilalamika__10__kwa gari letu na vijana wakora__11__kama askari polisi. Mbona tukadanganyika__12__jinsi hiyo? Muda si muda mmoja wa wale wezi__13__pale akitembea asteaste. Nilipigwa__14__. Alilia lakini kilio si dawa. Hatimaye akachomwa. __15__harufu ya nguo zikichomeka. Rafiki yangu aliyekuwa akiona njaa alitapika na kuzimia zi!

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | **A.** walicheka | **B.** walitucheka | **C.** walituchekea | **D.** walituchekelea |
| **9.** | **A.** kalulu | **B.** samaki | **C.** ng'ombe | **D.** fisi |
| **10.** | **A.** kuiba | **B.** kuibwa | **C.** kuibiwa | **D.** kuibia |
| **11.** | **A.** waliovaka | **B.** waliovalia | **C.** waliyavaa | **D.** waliojivaa |
| **12.** | **A.** rahisi | **B.** kirahisi | **C.** kiurahisi | **D.** virahisi |
| **13.** | **A.** akapita | **B.** wakapita | **C.** walipita | **D.** atapita |
| **14.** | **A.** kituta | **B.** kitoto | **C.** kitutu | **D.** kitute |
| **15.** | **A.** tuliona | **B.** tulisikia | **C.** tulihisi | **D.** tulinusa |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Ni maelezo yapi yasiyo sahihi?
A. Kiingilio ni pesa za kuruhusu kuingia mahali.
B. Nauli ni pesa unazotoa za usafiri.
C. Mahari ni pesa anazotoa bwana harusi.
D. Fidia ni pesa zinazotolewa mahakamani.

**17.** Ni sentensi gani haionyeshi matumizi sahihi ya "karibu"
A. Mwanahamisi atatutembelea hivi karibuni.
B. Alishambuliwa na majambazi karibu aage dunia.
C. Tulipofika karibu na mkahawa huo tulisikia mlipuko.
D. Kwaheri ndugu zangu. Haya karibu tena humu mwetu.

**18.** **"Ki" imetumikaje katika sentensi**
*Opore aliwasili alitupata tukiandika*
A. Kuonyesha masharti.
B. Kuonyesha hali ya kuendelea.
C. Kuonyesha hali ya kukanusha.
D. Kuonyesha hali ya udogo.

**19.** Chagua sentensi iliyoandikwa katika ngeli ya U-I
A. Mkono ambao ulikatika ulishonwa vizuri.
B. Mkunga aliyevuliwa atapikiwa wageni.
C. Gari la mkurugenzi huyo ni jipya.
D. Mbung'o husababisha ugonjwa wa malale.

**20.** Orodha gani iliyo na vivumishi tasa pekee?
A. Jipya, mizuri, mnene, jeupe.
B. Safi, dhaifu, hodari, shujaa.
C. Maridhawa, kamili, nyeusi, ghali.
D. Bora, duni, wengi, kidogo.

**21.** Kata ni katika ilhali toa ni kwa
A. toleana. B. toza.
C. tozwa. D. toweka.

**22.** Ni jawabu lipi lililo na maana sawa na maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii
*Mwalimu mkuu **alikata kalima** wakati mgeni wa heshima alipofika.*
A. Alionyesha hali ya furaha.
B. Alivumilia kero.
C. Alienda mahali pa siri.
D. Alikoma ghafla kuzungumza.

**23.** **Chagua usemi wa taarifa wa**
*"Mwalimu atawasili kesho jioni," baba alisema.*
A. Baba alisema kuwa mwalimu angewasili siku iliyofuata jioni.
B. Baba alisema kuwa mgeni angewasili kesho jioni.
C. Baba alisema kuwa mgeni atawasili siku iliyofuata jioni.
D. Baba alisema kuwa mgeni anawasili siku ijayo jioni.

**24.** **Ni upi udogo wa**
*Mguu wa ng'ombe umekatika*
A. Vijiguu vya vigombe vimekatika.
B. Maguu ya magombe yamekatika.
C. Kiguu cha kigombe kimekatika.
D. Guu la gombe limekatika.

**25.** $\frac{2}{9}$ kwa maneno ni
A. nusu tusui. B. tusui mbili.
C. tusui nusu. D. nusu tusui.

**26.** Tambua jina la makundi lisilofaa
A. Kidani cha barua.
B. Mzengwe wa wagomaji.
C. Ufefe wa mahindi.
D. Tanu ya chokaa.

**27.** Ni sentensi ipi iliyotumia kiunganishi ifaavyo?
A. Lau ya kuwa mwalimu mama ni mkulima.
B. Alimsaidia mathalani alikuwa na haja.
C. Aliishindia timu yake angaa ile aliyoiogopa sana.
D. Alienda kazini ingawa alikuwa mgonjwa.

**28.** Teua wingi wa' Hakumwamini mganga alipoitoa shingo ya mbuni.
A. Hawakuwaamini waganga walipoitoa shingo ya mbuni.
B. Hawakumwamini mganga alipozitoa shingo za mbuni.
C. Hawakuwaamini waganga walipozitoa shingo za mbuni.
D. Hakuamini waganga walipozitoa shingo za mabuni.

**29.** Maneno yaliyopigiwa mstari ni aina zipi za maneno?
*Magari yenyewe ni mazuri kuliko haya yaliyochakaa.*
A. Kitenzi, kivumishi, kielezi.
B. Kivumishi, kilinganishi, kiwakilishi.
C. Kiwakilishi, kivumishi, kiunganishi.
D. Kivumishi, kiunganishi, kielezi.

**30.** Watu waliooa kutoka familia moja huitwa
A. mitala. B. mwanyumba.
C. maumbu. D. mkemwenza.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Kwa siku za hivi karibuni, walimu na wazazi wamejionea mengi kutoka kwa watoto waliokuwa wamefunga shule kwa zaidi ya miezi mitatu. Wanafunzi hawa ni wale wa gredi ya nne waliosubiri kujiunga na gredi ya tano na wale waliokamilisha mtihani wao wa darasa la nane na kujiunga na kidato cha kwanza. Wanafunzi hawa walipokuwa nyumbani walijifunza na kuona mengi. Waliojifunza yalitokana na vifaa vya teknolojia mathalani mkono, vipakatalishi na hata televisheni. Si kweli kusema kuwa vifaa hivi vya teknolojia ni vibaya, lakini ni muhali kutaja kuwa vifaa hivi vimewapotosha watoto wengi na hata watu wazima.

Teknolojia imekuwa ni kama mvua ya masika. Licha ya kuimarisha maisha na kuyafanya kuwa ya manufaa zaidi, imeleta 'mbu' wanaotishia afya na maisha ya watumizi wayo. Nipe sikio kwa muda kiduchu nigusie mengi mazuri yaliyoletwa na teknolojia. Awali kabisa, teknolojia imerahisisha mawasiliano kwa kiwango kikubwa sana. Zipo eropleni na meli zinazoweza kujiendesha pekee kwa uangalizi wa nahodha bila ya kumchosha na usomaji wa ramani. Ndege yaweza kuwekwa katika hali ya kujiendesha huku rubani akiwa ametamalaki kwenye dungu.

Nyanja za afya nazo zilipewa kipaumbele na uvumbuzi huu wa teknolojia utafiti umefanywa na wataalam wengi kuhusu masuala ya maradhi hususan vyanzo, kinga na hata tiba mujarabu kupendekezwa. Madaktari wanaweza kusakura mtandaoni kutafuta maoni ya wenzao kuhusu baadhi ya mambo yenye utata, jambo ambalo limeimarisha huduma za afya pakubwa.

Naam! Asifuye mvua imemnyea. Siku hizi kukanyanga chechele na jambo tukizi kama mvua ya jangwani. Zipo ramani halisi kwenye mitandao ambazo kwa yakini huweza kumwelekeza msafiri kuelekea aendako hadi akafika. Inashangaza kuwa ata hospitali, maduka na hoteli almuradi kila utakapo utapapata kwenye ramani za mtandaoni.

Husemwa hakuna bamvua isiyokuwa na usubi. Aisee! Teknolojia ii hii ndiyo iliyoibua madhara si akali. Maadili ya watoto wetu yamekuwa hayasemeki wala kuandikika. Maadili ya watoto hawa yamemomonyolewa na mwigo wa tabia na itikadi za uzunguni. Ni wazi katika mitindo ya ajabu ya kimavazi tuionayo.

Wengi wa vijana hawa wabichi wamejipata wakishiriki vitendo vyenye fuska kwa kulaghaika kwa kuingia katika urafiki na watu wasiowajua. Uhusiano baina ya marafiki umevunjika kwa kusababishwa na mitandao ya jamii. Vijana, hawa wadogo, waliokamilisha masomo yao ya shule ya msingi na wale wenzao, wameonyesha bayana kuwa waliyojivunia wakiwa mbali na walimu, hayakuwa mambo ya kuwajenga, bali kuwabomoa.

Wazazi na washikadau wote, ninawasuta kuchukua hatua za mapema ili kuwaauni wanetu kabla hawajatokomea gizani. Heri kuzuia kuliko kuponya. Sote tuna wajibu wa kuwaelekeza wana hawa wasio be wala te. Wameghilibiwa tu kwa kudhani kuwa wanaenda na usasa lakini hawajui kuwa unaweza kuona mbele.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ni maelezo gani sahihi?
A. wanafunzi wote waliofanya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane, wamepotoka.
B. wanafunzi waliokaa nyumbani kwa muda mrefu walijiingiza katika vitendo visivyofaa.
C. ni wanafunzi wa gredi ya nne pekee walio tabia benibeni.
D. hakuna zuri walilojifunza wanafunzi hawa kutokana na teknolojia.

**32.** Masika na teknolojia yamefananishwa kwani
A. teknolojia imejaa mbu wengi yalivyo masika.
B. kando na masika teknolojia ina tija nyingi.
C. kama masika teknolojia ina madhara mengi.
D. yalivyo masika, teknolojia ina maadili mengi.

**33.** Neno 'mbu' limetumika katika habari: Halilengi
A. madhara ya teknolojia.
B. udhaifu wa teknolojia.
C. upungufu wa teknolojia.
D. faida za takenolojia.

**34.** Kutokana na teknolojia
A. ramani hazina faida kwenye ndege.
B. marubani wamekuwa wavivu zaidi.
C. eropleni inaweza kwenda yenyewe.
D. hakuna rubani aliye na kazi.

**35.** Kulingana na ufahamu, si sahihi kusema kuwa
A. teknolojia imeimarisha maenezi ya magonjwa.
B. teknolojia imeimarisha utafiti wa magonjwa.
C. teknolojia imeimarisha utafiti wa tiba za magonjwa.
D. teknolojia imeimarisha utafiti kuhusu vyanzo vya magonjwa.

**36.** Kulingana na ufahamu; Kabla ya daktari kutoa uamuzi wa jambo fulani yeye...
A. huangalia mtandaoni kujua maoni ya wengine.
B. huingia mtandaoni kuchunguza watakayo wengine.
C. huingia mtandaoni kuchunguza kashfa za wengine.
D. huingia mtandaoni kuwachunguza wenzake.

**37.** Methali; Aisifuye mvua imemnyea ina maana sawa na
A. hakuna masika yasiyokuwa na mbu.
B. alisifuye jua limemwangazia.
C. kilicho na mwanzo hakikosi kuwa na mwisho.
D. hakuna kizuri kisichokuwa na doa.

**38.** Mtu hawezi ***kukanyaga chechele*** siku hizi. Huku ni kumaanisha
A. mtu hawezi kukosa kutibiwa.
B. mtu hawezi kukosa kujua kuendesha ndege.
C. hakuna asiyeweza kujua dawa za magonjwa.
D. mtu hawezi kupotea njia.

**39.** Mwandishi anawahimiza wazazi na washikadau kufanya nini ili kuwaokoa watoto?
A. Wauwahi udongo ungali maji.
B. Wafanye bidii za mchwa.
C. Wafahamu kuwa jifya moja haliinjiki chungu.
D. Waadhibu watoto kwani zinguo la mtukutu ni ufito.

**40.** Anwani mwafaka ya makala haya ni
A. faida za teknolojia.
B. kazi ya teknolojia.
C. teknolojia na maisha.
D. hasara za teknolojia.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Kuwika kwa jogoo ndiko kulikonizindua kutoka usingizini. Nililitupa blanketi langu huko! Nikaamka na kuelekea bafuni kushtaki koga. Moyo ulinipapa kwani niliona kuwa wenzangu wangeiacha. Hata hivyo, nilifarijika nilipoitupia macho saa ya ukutani ambayo ilidai kuwa ilikuwa saa kumi kasorobo.

Nilirejea chumbani ambapo nilivaa upogoupogo. Nikaondoka nikizingatia kuwa chelewachelewa utampata mwana si wako. Kwa muda wa paka kunawia mate ama mbwa kukalia mkia wake, nilikuwa stanini mahali maalum ambapo tuliahidiana na kuafikiana tungekutana na wenzangu.

Kwa kweli ni mimi tu sikuwa nimewasili. Niliwakuta mori imewapanda. Lakini baada ya maongezi machache, walipoa maji. Kila mmoja wetu alikuwa amevalia sare rasmi ya polisi. Kusema kweli, ungetuona,

usingetuhumu kuwa tulikuwa majambazi sugu bali maafisa wa polisi. Kiongozi wetu Tembo alitupatia maagizo ya kulisubiri windo letu.

Tulisikiliza kwa makini ***tusije-tukakiuka kaida*** tulizostahili kuzifuata. Alitupanga barabara na kutuuliza, "Mko sawa?" Taabu!" Tulijibu kwa mkupuo. Zilikuwa zimesalia takriban dakika saba kala lodi tuliyemvizia awahi. Muda si muda, rukono ya Bosi wetu Tembo ilikiriza. Aliyepiga ni ndugu Nuru ambaye alikuwa akimwandama mkwasi yule bila ya yeye kujua. Alitutaka tukae ange kwani windo halikuwa na habari ng'o! kuwa lilisubiriwa kwa hamu na ghamu.

Na kwa kweli dakika zilipopita tatu, kwa umbali tuliona mwangaza angavu ukiangaza. Tulijua kuwa bila shaka, tajiri msubiriwa alikuwa amekutana na kifo chake ana kwa ana. Tulizitia silaha zetu tayari ili akijaribu kufanya ujeuri tumlaze chini na kumwua.

Gari lilikuja kwa machachari na makeke kana kwamba halikutaka kusimamishwa. Mie na "Askari" wenzangu, tulisimama katikati ya njia na kutoa ishara ya kusimama kama askari wa kawaida. Gari lilisimamishwa nasi tukaanza kumhangaisha dereva tukijua ndiye mwenye milioni hizo tatu tulizozitaka.

Lo! Tulizokuwa tumejilaghai! Aliyekuwa ameshikilia usukani alikuwa afisa wa polisi. Alitoka garini wanguwangu akaandamwa na wenzake. Aisee! Tulikuwa tumefumaniwa. Bwana Tembo alipojaribu kutoroka, do! Alipatwa na risasi mgongoni akajikuta chini. Tajiri alikuwa garini akijionea sinema ya bwerere. Kwa kuwa arubaini zetu zilikuwa zimefika, tulitiwa mbaroni huku Tembo akifikishwa korokoroni bila roho!

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, ni bayana kuwa
A. mwandishi alikuwa amelala usingizi mzito.
B. mwandishi alikuwa tayari kuanza kazi.
C. mwandishi alichanganyikiwa kutokana na mwiko wa jogoo.
D. mwandishi alikuwa na safari ya dharura.

**42.** Kuvaa upogoupogo ni kuvalia kwa namna gani?
A. Kuvaa kunakopendeza.
B. Kuvalia upesiupesi.
C. Kuvalia kivoloya na vibayavibaya.
D. Kuvaa polepole bila ya haraka.

**43.** Mwandishi alipofika walikoagana kupatana na wenzake
A. walikuwa na furaha tele.
B. walikuwa wamekasirika.
C. walikuwa wamehuzunika.
D. walikuwa na wasiwasi.

**44.** Sare rasmi za polisi walizovalia zilidhihirisha wazi kuwa
A. hao walikuwa walinda usalama rasmi.
B. waliujali usalama wa nchi na matajiri wake.
C. nguo za polisi huvaliwa na yeyote nchini.
D. wahalifu huvalia magwanda ya polisi ili kuwapumbaza watu.

**45.** Zilikuwa zimesalia takriban dakika saba kabla ya lodi aliyesubiriwa kufika. Dakika hizi zinaweza kuwa
A. 6 B. 7
C. 8 D. 4

**46.** Windo halikuwa na habari ng'o "Ni tamathali gani ya lugha iliyotumiwa katika nukuu hii?
A. Tashhisi.
B. Tanakali.
C. Tashbihi.
D. Kihisishi.

**47.** Mwandishi anasema, ***"tusije tukakiuka kaida,"*** yamepigiwa mstari. Ina maana kuwa
A. wasije wakapata hasara.
B. wasije wakatiwa nguvuni.
C. wasije wakafanya kinyume ya kawaida.
D. wasije wakayavuruga mambo.

**48.** Kulingana na ufahamu, ni sahihi kusema kuwa
A. wizi huleta utajiri wa haraka.
B. tajiri alituhumu hatari akasindikizwa na polisi.
C. askari hawakuwa wamejihami.
D. wezi hawakuwa na nia ya kumwua tajiri yule.

**49.** Gari lilikuja kwa makeke na machachari yaani lilikuja
A. kwa vishindo.
B. taratibu.
C. hahadhari.
D. kimya.

**50.** Hatima ya majambazi ni dhahiri kuwa
A. Mtende akutendaye.
B. Siku ya kufa kwa nyani miti yote huteleza.
C. Siku za mwizi ni arubaini.
D. Mwana mtukutu hali wali mkavu.